

## **Ashuru ni wapi?**

Ashuru ilikuwa ni nchi iliyokuwepo maeneo ya **Iraq, Uturuki, na Syria**.. Mataifa haya matatu yamechangia sehemu ya nchi hiyo ya Ashuru, kama vile mataifa matatu (*Kenya, Uganda na Tanzania*), yalivyo na sehemu katika ziwa Victoria, kadhalika na **Iraq, Uturuki na Syria** ni sehemu ya Taifa hilo liliokuwa linaitwa Ashuru.

Lakini kwasasa duniani hakuna Taifa linaloitwa **Ashuru**. Kwani baada ya mataifa hayo matatu kuzaliwa hilo la Ashuru likafa.

Na Uliokuwa mji mkuu wa Taifa la Ashuru, uliitwa **NINAWI**. Ninawi ndio mji Nabii Yona alioambiwa akahubiri Injili, lakini kinyume chake akakimbilia Tarshishi.. Kujua Ninawi ni wapi kwa sasa fungua hapa>**NINAWI**.

Vile vile kujua Tarshishi ni wapi kwasasa fungua hapa > **TARSHISHI**.

Asili ya Taifa la Ashuru kibiblia ni kutoka kwa Nimrodi..

*Mwanzo 10:8 "Kushi akamzaa Nimrodi, akaanza kuwa mtu hodari katika nchi.*

*9 Alikuwa hodari kuwinda wanyama mbele za Bwana. Kwa hiyo watu hunena, Kama Nimrodi, hodari wa kuwinda wanyama mbele za Bwana.*

*10 Mwanzo wa ufalme wake ulikuwa Babeli na Ereku, na Akadi, na Kalne, katika nchi ya Shinari.*

*11 Akatoka katika nchi ile akaenda mpaka Ashuru, akajenga Ninawi, na Rehoboth-iri, na Kala;*

*12 na Reseni, kati ya Ninawi na Kala, nao ni mji mkubwa".*

Lakini Taifa la Ashuru ndilo lililowachukua Israeli na kuwapeleka utumwani katika Taifa hilo. Lakini baadaye walirudi katika Taifa lao chini ya amri ya **Koreshi Mwajemi**.

Tafadhali washirikishe na wengine habari hizi njema,

Kwa maombezi/Ratiba za ibada/ Ushauri/ Maswali.

Piga namba hizi: +255693036618 au +255789001312

Pia kwa kupokea mafundisho ya kila siku kwa njia ya WHATSAPP, jiunge na channel yetu kwa kubofya link hii

>> <https://whatsapp.com/channel/0029VaBVhuA3WHTbKoz8jx10>

---

### **Mada Nyinginezo:**

### **Rudi nyumbani**

Share on:

WhatsApp